

**BODI YA NAFAKA NA MAZAO MCHINGANYIKO TANZANIA.**  
**VIGEZO VYA WAKALA**

---

**Wakala Mkubwa (Super Dealer).**

- a) Atapaswa kubainisha eneo atakalofanya kazi/biashara (Wilaya, Mkoa au Kanda).
- b) Awe na umri kuanzia miaka 18.
- c) Awe na mtaji wa kulipia walau tani thelathini (30).
- d) Awe na biashara halali inayotambuliwa na Mamlaka za Serikali ya Jamhuri ya Tanzania.
- e) Awe na ghalia (la kwake au la kukodi) lenye kukidhi matakwa ya ubora kwa ajili ya kuhifadhiha bidhaa kwa muda kabla ya kuzisambaza kwa Wateja.
- f) Awe na dhamana ya Benki kutoka Benki inayojulikana na kuaminika. (**Bank guarantee**).
- g) Awe na uwezo wa kulipa asilimia arobaini (40%) ya mzigo anaochukua kutoka Bodi na kumalizia malipo yanayobaki (60%) ndani ya wiki mbili (2) tangu achukue mzigo.
- h) Awe na uzoefu kwenye sekta ya nafaka kwa muda usiopungua mwaka mmoja ikiambatana na sifa njema kwenye eneo analofanya biashara/analoishi.
- i) Awe na miundo mbinu ya usambazaji wa bidhaa angalau yasipungue magari mawili(2).
- j) Awe na uwezo wa kutimiza majukumu ya kimkataba kwa ufanisi katika mazingira yote.
- k) Awe na historia ya mikopo isiyokuwa na shaka.

**Wakala Msambazaji (Distributors).**

- a. Awe na umri kuanzia miaka 18.
- b. Awe amebainisha eneo la kufanya biashara yake.
- c. Awe na eneo/duka la kwake au la kupanga.
- d. Awe na uwezo wa kulipa asilimia arobaini (40%) ya mzigo anaochukua kutoka Bodi na kumalizia malipo yanayobaki ndani ya wiki mbili (2) tangu achukue mzigo.
- e. Awe na biashara halali inayotambuliwa na Mamlaka za Serikali ya Jamhuri ya Tanzania. (Awe na TIN, Tax Clearance na Lesseni ya Biashara).

- f. Awe na uwezo wa kujieleza au Wafanyakazi wanaoweza kujieleza na kuelezea Taasisi na bidhaa.
  - g. Awe na miundo mbinu ya usambazaji wa bidhaa angalau yasipungue magari mawili (2).
  - h. Awe na ghal (la kwake au la kukodi) lenye kukidhi matakwa ya ubora kwa ajili ya kuhifadhiya bidhaa kwa muda kabla ya kuzisambaza kwa Wateja.
  - i. Awe na mtandao wa Wateja kwa ajili ya kuwasambazia bidhaa.
  - j. Awe na mtaji unaoanzia milioni kumi (Tzs. 10,000,000/=).
  - k. Awe na historia ya uaminifu isiyo na shaka.
  - l. Awe na uwezo wa kutimiza majukumu ya kimkataba kwa ufanisi katika mazingira yote.
- 

**Wakala Dalali (Commission agents).**

- a. Awe na umri kuanzia miaka 18.
  - b. Awe na kitambulisho kinachomtambulisha kama NIDA, Leseni, Leseni ya udereva etc.
  - c. Awe na utambulisho kutoka Serikali ya Mtaa anakoishi.
  - d. Awe na Mdhamsini Mkazi na mwenye mali isiyohamishika au Mtumishi wa umma.
  - e. Awe na mwenendo unaokubalika kwenye jamii anayoishi na hajawahi kufungwa jela kwa kosa lolote la jinai.
  - f. Awe anatambuliwa na Serikali na mamlaka za kodi. (awe na TIN).
  - g. Awe na uwezo wa kujieleza na kuelezea Taasisi na bidhaa zake.
  - h. Awe na uwezo wa kutimiza majukumu ya kimkataba kwa ufanisi katika mazingira yote.
- 

